

Tuma rejesho ya kodi ili urejeshewe pesa



Unaweza kustahiki maelfu ya dola katika kurejeshewa kodi yako unapodai Federal Earned Income Tax Credit na Child Tax Credit

Jinsi ya kupata mikopo yako ya kodi:

- 1 Angalia kama unahitimu**
Jua ni kiasi gani unaweza kupokea katika [TaxOutreach.org/TaxCredits](https://www.TaxOutreach.org/TaxCredits).
- 2 Pata usaidizi wa kodi BILA MALIPO**
Nenda kwa [GetYourRefund.org](https://www.GetYourRefund.org) au piga simu kwa 800-906-9887, hata kama huwa hutoi kodi.
- 3 Toa kodi kodi zako**
Pata usaidizi bila malipo wa kurejesha kodi kabla ya tarehe 1 Oktoba, 2023.

Nini cha kuleta kwa uteuzi wa ushuru:

- Kitambulisho halali cha picha
- Kadi ya usalama wa jamii, barua ya uthibitishaji ya nambari ya usalama wa jamii, au ITIN kwa kila mtu kwenye malipo yako ya kodi
- Fomu za W-2 au 1099
- Fomu 1095-A
- Arifa zozote za IRS
- Marejesho ya ushuru wa mwaka 2020 na 2021, ikiwa unayo
- Pin ya ulinzi wa kitambulisho (IP PIN), ikiwa unayo



Kwa maelezo zaidi, nenda kwa [TaxOutreach.org/TaxCredits](https://www.TaxOutreach.org/TaxCredits) au piga simu IRS kwa 1-800-829-1040



Kustahiki Earned Income Tax Credit (EITC) na Child Tax Credit (CTC)

Ikiwa huna watoto unaweza kufuzu kwa EITC ya hadi \$560 ikiwa:

Umri:

Ulikuwa na umri wa kati ya miaka 25-64 tarehe 31 Disemba, 2022.

Mapato ya mwaka 2022:

Umeapata chini ya \$16,480 (\$22,610 ikiwa umeolewa).

Ikiwa wewe si raia wa marekani unaweza kuhitimu ikiwa:

► **EITC:** Wewe, mpenzi wako, na motto yeyote anayedai ana nambari halali ya usalama wa jamii (SSN).

► **CTC:** Mtoto yeyote anayedai ana SSN. Wewe na mpenzi wako lazima muwe na SSN au nambari ya utambulisho ya mlipakodi binafsi (ITIN).

Je, ninahitimu?

Wakati wa kodi, unaweza kudaiwa kodi kidogo na urejeshewe pesa na Earned Income Tax Credit na Child Tax Credit Iwapo ulifanya kazi mwaka wa 2022, unaweza kustahiki mikopo hii.

Manufaa ya umma:

- Kudai masalio haya ya kodi hakutabadilisha ustahiki wako wa manufaa ya shirikisho kama vile SNAP (mihuri ya chakula), SSI, Medicaid, usaidizi wa pesa au makazi ya umma.
- Ukihifadhi marejesho ya kodi yako, haitahesabiwa dhidi ya vikomo vya mpango wa manufaa unaofadhiliwa na serikali kwa miezi 12 baada ya kurejesha pesa.

Ikiwa una watoto unaweza kufuzu kwa EITC na CTC ikiwa:

Ukaazi:

► Watoto wako waliishi nawe kwa zaidi ya nusu ya mwaka 2022.

Umri – watoto lazima wawe:

► **EITC:** 18 au chini mnamo 31 Disemba, 2022 (wanafunzi wa wakati wowote wanaweza kuwa chini ya miaka 24 na watoto walio na ulemavu wanaweza kuwa na umri wowote).

► **CTC:** 16 au chini mnamo 31 Disemba, 2022.

Mapato ya mwaka 2022:

► **Kwa Federal CTC**, ikiwa ulipata zaidi ya \$2,500, unaweza kudai salio hadi \$2,000 kwa kila motto.

► **Kwa Federal EITC**, mapato yako lazima yaw echini ya vikomo vifuatavyo:

Idadi ya watoto	Wafanyakazi wasioolewa na mapato chini ya:	Wafanyakazi walioolewa na mapato chini ya:	EITC hadi:
Mtoto 1	\$43,492	\$49,622	\$3,733
Watoto 2	\$49,399	\$55,529	\$6,164
Watoto 3 au zaidi	\$53,057	\$59,187	\$6,935

Hujachelewa kudai mikopo iliyopanuliwa ya mwaka 2021!

Kwa sababu ya janga hili, Mikopo ya EITC na Child Tax Credit ilipanuliwa na kupatikana kwa watu wengi zaidi. Upanuzi huo umeisha, Lakini ikiwa ulistahiki EITC iliyopanuliwa ya mwaka 2021, Child Tax Credit lililopanuliwa la mwaka 2021, au awamu zozote tatu za ukaguzi wa vichocho na hukuzidai, bado haujachelewa! Tembelea TaxOutreach.org/expanded ili kupata maelezo zaidi.